# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## CHUO CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI - KARAGWE DVTC


S.L.P. 62
KARAGWE.


Unapojibu tafadhali taja
Kumb. Na. VETA/KRG/DVTC/UF.

.........................................
.........................................
.........................................

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI CHUO CHA KARAGWE DVTC - HATUA YA KWANZA**

**1. MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**

i. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika Fani ya ______________________________________ katika ngazi ya kwanza (Level I) kwa masomo ya **kutwa/bweni**

ii. Mafunzo yatachukua muda wa mwaka mmoja (kuanzia mwezi January 2025 mpaka Desemba 2026

iii. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe 12/01/2025.

iv. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa.

v. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa.

vi. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua.

vii. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo.

viii. Unatakiwa kununua vifaa vilivyoambatanishwa na barua hii kwa matumizi yako chuoni.

ix. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyoambatanishwa na barua hii.

x. Hutapokelewa chuoni iwapo utafika bila kutimiza maitaji yote yaliyotajwa. Lipa mapema ili uweze kusajiliwa.

xi. Nafasi yako itapotea kama utashindwa kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo.

## 2. ADA NA GHARAMA NYINGINE

| NA | MCHANGANUO WA MALIPO | KUTWA | BWENI |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada | 60,000 | 120,000 |
| 2 | Tahadhari | 20,000 | 20,000 |
| 3 | Michezo | 20,000 | 20,000 |
| 4 | Vifaa vya usafi | 10,000 | 10,000 |
| 5 | Sare: Suruali 2, Overlori/overkoti 1 | 65,000 | 65,000 |
| 6 | Kitambulisho | 5000 | 5000 |
| 7 | Nembo ya VETA | 5000 | 5000 |
| 8 | T-shirt ya VETA | 20,000 | 20,000 |
| 9 | Bima ya Afya | 50,400 | 50,400 |
| 10 | Maahafari | 20,000 | 20,000 |
| | **JUMLA KUU** | **270,400** | **335,400** |

Malipo yote yafanyike kupitia Control No. Fedha za bima ya afya zitalipwa ofisi ya uhasibu tu.

**NB. UTARATIBU WA JINSI YA KUFANYA MALIPO UTAPEWA NA MHASIBU WA CHUO MARA TU BAADA YA KURIPOTI CHUONI.**

## 3. MAHITAJI MENGINE

Pia kila mwanafunzi anatakiwa awe na vifaa vifuatavyo na avionyeshe kabla ya kuanza masomo;

i. Jozi moja ya viatu vya usalama (Safety Boot siku ya Practical)
ii. Vifaa vya hesabu (Mathematical Set)
iii. Soksi nyeupe
iv. Ream (Photocopy Paper A4)
v. Madaftari makubwa (3Q) nane (8).
vi. Shati mbili za rangi nyeupe pamoja na sweta ya blue yenye V shape

4. Wanafunzi wa Bweni wanatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo vitakavyowezesha kuishi chuoni.

i. Vyombo vya chakula- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
ii. Godoro linapatikana chuoni kwa gharama ya shilingi 20,000 tu kwa mwaka.
iii. Ndoo na beseni vya kuchotea maji na kuogea Pamoja na vifaa vingine vya usafi binafsi kama sabuni, miswaki na dawa za meno.

MKUU WA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI WILAYA KARAGWE

.............................

**Agnes Louis Qorro**
**MKUU WA CHUO**

**SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI**

ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI STADI KILA MWANACHUO ANATAKIWA KUZINGATIA NA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:

1. MAHUDHURIO:

- Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii inamaana ifikapo saa 1:30 wanafunzi wote wawe wamefika chuoni. ADHABU KALI ITATOLEWA KWA WACHELEWAJI
- Mwanafunzi harusiwi kutoka nje ya chuo Kwenda nyumbani, hospitalini au sehemu yeyote ile bila ruhusa na mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa.
- Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima taarifa zifike chuoni bila ya kufanya hivyo ni kosa la kinidhamu
- Mahudhurio chini ya 80% mwanafunzi hatoruhusiwa kufanya mitihani ya TAIFA.
- Ni marufuku wanachuo wa kutwa na wa bweni kuingia mabwenini muda wa vipindi ikibainika atachukuliwa hatua kali

2. MAVAZI

- Sare ya chuo ni suruali ya dark bluu na shati jeupe mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo itavaliwa wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani na wakati wote shati liwe limechomekewa.
- Ovaroli litavaliwa wakati wa vipindi vya vitendo tu (practical)
- Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) haziruhusiwi kuvaliwa chuoni.
- Mwanafunzi yeyote hatorusiwa kutoka nje ya bila kuvaa sare ya chuo.

3. USAFI WA MWILI

- Hairusiwi kuvaa heleni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo. Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.
- Nywere kwa wavula: zikatwe ziwe fupi na kipara na ndevu haviruhusiwi kabisa
- Nywere kwa wasichana: zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni)
- Kucha zisifugwe kabisa wala kupakwa rangi

4. WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:

- ✓ Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja.
- ✓ Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.
- ✓ Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyokuwa ndani ya chuo.
- ✓ Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. UGOMVI:
Ugomvi kupigana au kushambuliana ni kosa la jinai. Atakayebainika akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa Kwenye vyombo vya dola.

6. MAHUSIANO YA KIMAPENZI:

- Iwapo itabainika kuna mahusiano ya kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafunzi wote wawili mtasitishwa masomo.
- Mwanafunzi wa kiume au kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila kibali au ruhusa.

7. MIGOMO:
Migomo ni marufuku, kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

8. LUGHA
Lugha inayotumika kuendeleshea mafunzo ni kiingiereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.

9. ULEVI.
Iwapo itabainika unatumia kilevi chochote uwapo chuoni uongozi wa chuo utalazimika kufukuza chuo.

## SHERIA ZA NYONGEZA KWA WANACHUO WA BWENI

i. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho kutoka kwa afisa TEHAMA, Mratibu wa mafunzo na ajulishwe mkuu wa chuo mara moja.

ii. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi

iii. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya chuo siku zifuatavyo:
- Jumapili tangu saa 12:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni
- Jumamosi tangu saa 4:00 mchana hadi saa 11:00 jioni
- Hairusiwi kutoka nje chuo wakati wowote bila kibali maalum

iv. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo au kufukuzwa kabisa.

v. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha chuo na atajiandikisha langu kuu na sare ya chuo. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya chuo bila kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni Pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni.

vi. Hairusiwi kupikia chakula bwenini na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua
- Ni marufuku wanachuo wa kiume na kike kutembeleana mabwenini
- Hairuhusiwi kupeleka KABISA kwa wanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa chuo bila ruhusa au kibali maalumu

vii. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.

viii. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 za usiku.

ix. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo, ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo
- Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila jumamosi kuanzia saa 4:00 mchana hadi saa 11:00 jioni
- Kila jumapili na siku za siku za sikukuu kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni

x. Vyumba/madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo

xi. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya chuo itatolewa na ofisi ya Mkuu wa chuo.

xii. Ruhusa ya kutoka chuoni Jumamosi saa 4:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni Jumapili na siku za sikukuu saa 4:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Majina yaandikwe Kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mhusika aweke muda wa kutoka na kusaini arudipo.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na namba zifuatazo **+255 744 974 537**
**Kaimu Mratibu wa Mafunzo**

*VET MED FORM - IE*

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY (VETA)

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**The Medical Officer**

**Government Hospital/Dispensary**

…......................................

…......................................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

**NAME**.........................................................................

Please examine the above-named trainee to certify his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an.........................................

i. Eyesight:.....................................

ii. Hearing:....................................................

iii. Asthma:......................................................

iv. Epilepsy:......................................................

v. Other serious diseases:..............................

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I have examined the above-named trainee and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above:

**Date**................. **Designation**................. **Signature**....................

**& Official stamp**

**NAFASI YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**MWANACHUO**

Mimi.................................................................. Ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa na nitazingatia sheria na kanuni za chuo.

Sahihi................................................ Tarehe ...........................

**MDHAMINI**

Mimi ......................................... S.L.P ................................ Ninathibitisha kuwa ninamdhamini ................................................... Na nitalimlipia gharama zote za mafunzo (ada) pamoja na nauli wakati wote wa kwenda chuoni nakurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo.

**Sahihi.................................... Tarehe .......................................**